bitesize

RESOURCE & SUPPORT HUB

**Kuelewa unyonyaji, dhuluma na unyanyasaji wa kingono (SEAH) na ukatili wa kijinsia (GBV)**

Unyonyaji, dhuluma na unyanyasaji wa kingono (SEAH) na ukatili wa kijinsia (GBV) una uhusiano wa karibu lakini ni maeneo tofauti ya kazi, hasa ndani ya sekta ya maendeleo na ya kibinadamu.

Mashirika ya Kijamii, Wafadhili, Serikali, Taasisi za Kifedha za Kimataifa na mashirika mengine yote yanaweza kuwa na ufafanuzi tofauti wa SEAH na ukatili wa kijinsia (GBV). Hata hivyo, ni muhimu kwa watendaji kuelewa tofauti za kinadharia na vitendo na kufanana kati ya haya maeneo mawili ya kazi. Kuhakikisha kuwa kazi yetu kama watendaji inategemea uelewa kamili wa hili mwishowe utasababisha kuimarishwa kwa kazi ya kuzuia, kupunguza na kuitikia ndani ya sekta hii.

| Unyonyaji, Dhuluma na Unyanyasaji wa Kingono (SEAH) | Ukatili wa Kijinsia (GBV) |
| --- | --- |
| **Ufafanuzi** | |
| SEAH ni neno linalotumiwa kuashiria unyonyaji, dhuluma na unyanyasaji wa kingono. Ingawa unyonyaji, dhuluma na unyanyasaji wa kingono unaweza kutokea mahali popote katika jamii, wakati unatumiwa kama neno linalojumlisha katika sekta ya maendeleo na kibinadamu, neno hilo linamaanisha SEAH inayofanywa na wale wafanyakazi ndani ya, au na, mashirika ya maendeleo na kibinadamu na ndani ya Misheni za Kulinda Amani.<br><br>Maneno husika ndani ya SEAH yamefafanuliwa [kwenye tovuti ya Kituo cha Rasilimali na Usaidizi (RSH)](#).<br><br>SEAH kwa kawaida hutokea katika mazingira ya kazi, au mazingira yanayohusiana na kazi, ikijumuisha mazingira ya programu au usafiri wa kazi. | "Ukatili wa kijinsia" ni neno jumlishi la kitendo chochote chenye madhara ambacho kinafanywa kinyume na mapenzi ya mtu na kulingana na tofauti ya mazoea ya jamiihusika (kwa mfano jinsia) kati ya wanaume na wanawake. Inajumuisha vitendo vinavyosababisha madhara ya kimwili, kingono au kiakili au mateso, vitisho vya vitendo hivyo, kulazimishwa na kunyimwa uhuru. Vitendo hivi vinaweza kutokea kwa umma au kwa faragha.<br><br>Neno "Ukatili wa kijinsia (GBV)" hutumiwa sana kusisitiza jinsi ukosefu wa usawa wa kimfumo kati ya wanaume na wanawake, ambao upo katika kila jamii ulimwenguni, hufanya kazi kama sifa ya kuunganisha na ya kimsingi ya aina nyingi za ukatili unaofanywa dhidi ya wanawake na wasichana. Neno "ukatili wa kijinsia" pia linajumuisha ngono ukatili uliofanywa kwa lengo la wazi la |

Ndani ya sekta ya maendeleo na ya kibinadamu, SEAH ni sehemu ya kanuni za maadili ya shirika. Kanuni ya maadili inashughulikia mwenendo katika maisha ya kitaaluma na maisha ya kibinafsi - wafanyakazi wanatambuliwa kuwa sehemu ya shirika na mazingira yanayohusiana na kazi yanaweza kuwa nje ya ofisi sawia na wakiwa ofisini.

Watuwalio katika hatari ya SEAH ni watumiaji wa huduma za shirika, wanachama wa jamii au wafanyakazi.

kuimarisha kanuni za usawa wa kijinsia za kiume na za kike.[1]

Ni muhimu kutambua kwamba wanaume, wanawake, wavulana na wasichana wote wanaweza kupitia ukatili, lakini hadi sasa utafiti wa ukatili wa kijinsia (GBV), sera na programu kwa kiasi kikubwa imezingatia wanawake na wasichana, kama usawa wa kijinsia wa kimiundo na kimfumo unawapendelea wanaume wenye mamlaka makubwa na rasilimali ambazo hufanya wanawake na wasichana kuwa katika hatari kubwa ya madhara.

Ukatili wa kijinsia (GBV) unaweza kutokea mahali popote.

| Unyonyaji, Dhuluma na Unyanyasaji wa Kingono (SEAH) | Ukatili wa kijinsia (GBV) |
|---|---|
| **Sababu ni nini?** | |
| SEAH inaweza kuongozwa na aina tofauti za matumizi mabaya ya [madaraka](#) na ukosefu wa usawa.<br><br>Madaraka zaidi ambayo mtu anayo, fursa kubwa anayo ya kuwanyonya, kuwadhulumu na kuwanyanyasa wengine. Madaraka kidogo ambayo mtu anayo, zaidi wanaweza kulengwa kwa unyonyaji, dhuluma na unyanyasaji. Kiwango cha madaraka aliconacho mtu kimehusishwa kwa karibu na mambo ya kimiundo, uongozi na hali:<br><br>• Ukosefu wa usawa wa miundo unaohusishwa na kwa mfano jinsia, rangi, ukabila, hali ya ulemavu, utambulisho wa kijinsia, mwelekeo wa kijinsia, darasa, tabaka.<br>• Uongozi ndani ya mashirika, kwa mfano, kati ya wafanyakazi wasimamizi na wafanyakazi wa kiwango cha chini wa kimataifa na wa kitaifa.<br>• Sababu za kihali, kwa mfano, mfanyakazi wa kibinadamu mwenye madaraka ya kuamua upatikanaji wa msaada wa kibinadamu, kama vile chakula au pesa au vocha.<br><br>Wanawake na wasichana wana uwezekano mkubwa wa kulengwa kwa SEAH kwa sababu ya ukosefu wa usawa wa kijinsia wa kimiundo na kimfumo ambao unawapendelea wanaume na kuwapa madaraka makubwa na rasilimali. | Ukatili wa kijinsia daima unategemea ukosefu wa usawa wa kijinsia na tofauti za kijamii kati ya wanaume na wanawake. Kulengwa kwa Ukatili wa kijinsia kunaweza kuzidishwa mtu anakabiliwa na aina nyingi za ukosefu wa usawa.<br><br>Kwa vile SEAH mara nyingi hufanywa dhidi ya wanawake na wasichana, mara nyingi huchukuliwa kuwa aina ya Ukatili wa kijinsia. Hata hivyo, *inaweza kuwa si aina ya Ukatili wa Kijinsia kila wakati*.<br><br>Ukatili wa kingono unaweza kufanywa kulingana na masuala mengine ya ukosefu wa usawa. Kwa mfano, ambapo mwanamke ambaye mfanyakazi wa kimataifa anamnyanyasa kingono mfanyakazi wa kiwango cha chini ambaye ni wa kitaifa. Katika mfano huu, unyanyasaji hautokani na ukosefu wa usawa wa kijinsia na ubaguzi wa kijinsia, ila una mizizi ya kanuni za kitamaduni zenye madhara zinazohusiana na utaifa, rangi na ukoloni. Ukatili wa kingono unaofanywa dhidi ya mwanaume mwenye ulemavu unaweza kutokana na ulemavu huo kama njia ya ubaguzi. |

| Unyonyaji, Dhuluma na Unyanyasaji wa Kingono (SEAH) | Ukatili wa kijinsia (GBV) |
|---|---|
| **Wahalifu wakuu ni kina nani?** | |
| SEAH hufanywa na wafanyakazi au wawakilishi kutoka kwa Mashirika ya Kijamii.<br><br>Wahalifu wengi huwa wanaume, ingawa hii sio wakati wote. Wahalifu wengi ni watu wenye madaraka makubwa ya kimiundo, uongozi na/au kihali kuliko waathirika. | Ukatili wa kijinsia kwa kimsingi, lakini sio kila wakati, hufanywa na wanaume. |
| **Waathiriwa au manusura ni kina nani?** | |
| Wafanyakazi wa Mashirika ya Kijamii, wawakilishi na mwanachama yeyote wa jamii ambaye anaingiliana na Shirika la Kijamii, anaweza kuwa katika hatari ya SEAH.<br><br>Wanawake na wasichana wako hatarini zaidi. Ukosefu wa usawa wa kijinsia sio sababu kila wakati, hata hivyo na watoto, watu wenye ulemavu na watu wanaokabiliwa na aina nyingine za ubaguzi pia wanaweza kulengwa. Watu wanaweza kuwa katika hatari kubwa ya kulengwa kwa SEAH kwani wao hupitia ukosefu wa usawa unaoingiliana. Wasichana, kwa mfano, wako katika hatari kubwa kutokana na toauti za umri na zinazohusiana na uwezo wa kijinsia. | Wanawake na wasichana wako katika hatari zaidi ya Ukatili wa kijinsia. Watendaji wa Ukatili wa kijinsia mara nyingi huangazia wanawake na wasichana katika muitikio wao kwa Ukatili wa kijinsia kutokana na ukosefu wa usawa wa kijinsia na kimfumo na ubaguzi unaosababisha hatari yao kubwa iliyoratibiwa ya Ukatili wa kijinsia.<br><br>Katika baadhi ya matukio, wanaume na wavulana wanaweza pia kuwa manusura wa Ukatili wa kijinsia. Kwa mfano, katika hali za migogoro, ukatili wa kijinsia wakati mwingine hufanywa na wanaume dhidi ya wanaume na wavulana wengine kwa lengo la kuwaiga na kuwaaibisha. |
| **Hatari hizi zinaingiliana kwa njia gani?** | |

Mtu yeyote aliye na aina moja au zaidi ya ukosefu wa usawa =

hatari kubwa ya SEAH Wanawake/msichana = hatari kubwa zaidi

ya SEAH au Ukatili wa Kijinsia

Wanawake / msichana + ukosefu mwingine wa usawa = hatari kubwa ya SEAH au Ukatili wa Kijinsia

# Jinsi mashirika yanashughulikia SEAH

⇨ Wafanyakazi wote na wawakilishi wana jukumu la kuzuia na kuitikia SEAH. Inahitaji juhudi nzima la kimashirika na ni kipengele cha utamaduni wa kimashirika. Wafanyakazi wengine wana majukumu zaidi, kwa mfano wafanyakazi waandamizi, wafanyakazi wa Rasilimali Watu, wafanyakazi wanaotembelea maeneo ya programu.

⇨ Hatua za SEAH hulenga kuzuia na kuitikia katika shirika lote; na kwa kiwango cha chini kwa ujumla inajumuisha:

- Kutengeneza na kudumisha sera na taratibu husika
- Udhibiti wa Hatari za SEAH
- Uajiri ulio salama na mafunzo ya mara kwa mara kwa wafanyakazi
- Kuunda utamaduni wa kimashirika unaoelewa na kutoa changamoto katika kutokea kwa SEAH
- Kuunda utamaduni wa kimashirika unaoelewa na kutoa changamoto katika ukosefu wa usawa wa kijinsia, ukosefu wa usawa wa rangi na masuala mengine ya uanuwaina usawa
- Kutengeneza mfumo kwa wote wa kuripoti dhuluma na la shirika kuitikia
- Kujiandaa kwa ajili ya kusimamia uchunguzi pale inapohitajika
- Kubuni na kutoa programu salama

Kulinda usalama na Ulinzi kutokana na Unyonyaji, Dhuluma na Unyanyasaji wa Kingono(PSEAH) ni maneno yanayoeleza hatua baina ya mashirika ya kushughulikia SEAH.

Neno kulinda usalama kwa ujumla linajumuisha madhara mengine yasiyo ya kingono na dhuluma.

Neno Ulinzi dhidi ya Unyonyaji, Dhuluma na Unyanyasaji wa Kingono (PSEA) pia huashiria hatua zinazochukuliwa ili kuwalinda watu dhidi ya kufanyiwa unyonyaji wa kingono na dhuluma na wafanyakazi na programu. Tofauti na SEAH, PSEA haijumuishi unyanyasaji wa kingono.

# Jinsi mashirika yanashughulikia Ukatili wa kijinsia

⇨ Kazi ya kuzuia na kuitikia Ukatili wa kijinsia kawaida ni mpango katika programu na / au mradi wa utetezi. Inapaswa kuongozwa na wataalamu wa Ukatili wa kijinsia na kazi ya kuitikia (hasa) inapaswa kuongozwa na wanawake na wasichana.

⇨ Programu za Ukatili wa kijinsia zimeundwa na kutolewa ili kulinda watu kwa kushughulikia wanaotekeleza na kuitikia matukio ya Ukatili wa kijinsia. Pia, malengo ya Ukatili wa kijinsia yanaweza kuunganishwa katika programu zingine, kwa mfano mipango ya elimu, lishe au ulinzi wa kijamii.

⇨ Miongoni mwa mambo mengine, programu bora dhidi ya Ukatili wa kijinsia au malengo yanajumuisha:

- Mtazamo wa sekta mtambuko na wa njia ya huduma mbalimbali ya kuitikia mahitaji mbalimbali ya mtu binafsi au kikundi, ikijumuisha ya waathiriwa na manusura
- Kuanzisha mifumo ya kuripoti unyanyasaji, kuitikia na kutoa rufaa hadi kwa huduma muhimu
- Programu ambazo zinategemea uelewa wa kimazingira na kufanya kazi kwa karibu na wanachama wote wa jamii
- Uanaharakati wa miaka mingi na mkuu katika jamii ili kubadili mitazamo hatari ya kijinsia, majukumu na mazoea ya jamii
- Wafanyakazi na wawakilishi ambao wanachaguliwa kufuatia mtazamo wao kuhusu jinsia na tabia isiyo ya vurugu

Soma hapa zaidikwa habari kuhusu kile kinachofanya kazi katika kuzuia ukatili dhidi ya wanawake na wasichana.

[1] Kamati ya Kudumu ya Asasi Mbalimbali (IASC), 2015a. Miongozo ya Kuunganisha Hatua za Ukatili wa Kijinsia katika Mikakati ya Hatua za Kibinadamu: Kupunguza hatari, kukuza ujasiri na kusaidia kupona, uk. 3